Mwongozo wa ITU

Kuhusu jinsi ya kuhakikisha kuwa maelezo, huduma na bidhaa za kidijitali zinafikiwa na watu wote, wakiwemo Watu wenye Ulemavu wakati huu wa COVID-19[i]

Ulimwengu unakabiliwa na hali ibuka ambapo Teknolojia ya Habari ya Mawasiliano imeelekea kuwa njia ya pekee ya watu kuwasiliana. Jamii haijawahi kukabiliwa na hali kama hii ya kutegemea mifumo ya kidijitali kupata habari, huduma au bidhaa muhimu zinazohitajika ili kusitawi. Hivyo, kufikia maelezo na maagizo wakati huu wa janga la COVID-19 ni muhimu kwa watu wote, bila kujali jinsia, uwezo, umri au eneo.

Kwa sababu hii, inafaa maelezo muhimu ya kidijitali kuhusu COVID-19 yasambazwe na yatolewe kwa njia[1] zinazoweza kufikiwa kwa urahisi ili kuhakikisha kuwa yamewafikia watu wote na kuwa hakuna atakayeachwa nyuma, wakiwemo watu wenye ulemavu, hasa walio na matatizo ya kuona au kusikia na wanahitaji zana maalum kama vile visoma skrini, manukuu au lugha ya ishara ili waweze kusoma na kuelewa maelezo ya kidijitali. Kama sivyo, watu wengi wenye ulemavu watakuwa katika hatari kubwa ya kuambukizwa kutokana na kutopata maelezo kuhusu tahadhari za kuzingatia wakati wa janga hili.

Hivyo, ni muhimu sana kutumia njia mbambali za mawasiliano zinazoweza kufikiwa kwa urahisi kama vile tovuti, simu, redio, video, vijikaratasi, manukuu, gumzo, nk. pamoja na kutoa maelezo kwa lugha ya kawaida, iliyo rahisi kusoma na kwa njia zinazoweza kufikiwa na watu wenye ulemavu. Kutoa na kuhamisha jamii kuhusu nambari maalum za usaidizi ambazo madhumuni yake ni kuhakikisha kuwa maelezo kuhusu afya ya umma yanafikiwa (ikijumuisha huduma kwa wasiosikia na wenye matatizo ya kusikia) ni muhimu katika kuzuia msambao na athari za janga hili linalokabili ulimwengu.

Watu wengi wenye ulemavu wanategemea kuletewa bidhaa muhimu nyumbani mara kwa mara ili kulinda maslahi yao kama vile madawa, chakula na bidhaa za usafi. Hivyo, pamoja na athari chanya ambazo zimesababishwa na kutotangamana kwa ukaribu na kuathirika kwa shughuli za kijamii, ikiwa wauzaji na watoa huduma na bidhaa za afya, pamoja na mashirika mengine muhimu hayatahakikisha kuwa maelezo, huduma na bidhaa wanazotoa mtandaoni zinafikiwa

---

[1] **Video za mafunzo za ITU kuhusu jinsi ya kuandaa na kufanya maudhui ya kidijitali yafikiwe kwa urahisi**

Pata kozi za binafsi za ITU- D za ufikiaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano zinazotolewa mtandaoni bila malipo kwenye viungo vifuatavyo:

- *Ufikiaji wa Teknolojia ya Habari na Mwasiliano - Ufunguo wa mawasiliano kwa watu wote*
- ***Ufikiaji wa Wavuti – Msingi wa Jumuiya ya Kidijitali Inayojumuisha Watu Wote***

na watu wote, wengi walio na ulemavu hawataathirika tu bali maisha yao yatakuwa hatarini, kutokana na kutopata maelezo, madawa, bidhaa na huduma zingine muhimu wanazohitaji.

Kutokana na mchango mkubwa wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika janga la COVID-19 linalokabili ulimwengu mzima, mwongozo ufuatao unatoa maelezo na hatua muhimu zitakazohakikisha kuwa maelezo, huduma na bidhaa za kidijitali zinazotolewa kote ulimwenguni zinafikiwa na watu wote wakiwemo Watu wenye Ulemavu, na kuwa hakuna atakayeachwa nyuma katika vita dhidi ya janga hili linalokabili ulimwengu.

MAELEZO NA HATUA MUHIMU

1. **Hakikisha kuwa maelezo, huduma na masharti muhimu yanayotolewa kidijitali kuhusu kupunguza kusambaa kwa COVID-19 yametolewa kwa njia mbalimbali ili watu wote wakiwemo watu wenye ulemavu waweze kufikia maelezo haya muhimu:**

Maudhui na maelezo kuhusu COVID-19 sharti yatolewe kwa njia mbalimbali ili yaweze kufikia kila mtu, wakiwemo watu wenye ulemavu. Kwa mfano, matangazo ya umma kwenye televisheni, video za mtandaoni na mtiririko wa moja kwa moja wa sauti pekee hazitaweza kuwafikia watu wenye matatizo ya kusikia isipokuwa zijumuishe manukuu au ukalimani wa lugha ya ishara. Sawa na hali nyingine yoyote ya dharura, kando na vyombo vya habari vya kawaida (Televisheni na redio), ulimwengu wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano unajumuisha njia anuwai zinazowawezesha watu wenye ulemavu kufikia habari katika hali zisizo za kawaida kama sasa: simu za waya, sauti kwenye simu ya mkononi, SMS au ujumbe wa maandishi, na huduma na nyenzo za mtandaoni kama vile tovuti, video, programu za kutuma ujumbe papo hapo, huduma za sauti kwenye Itifaki ya Intaneti (IP), mitandao ya kijamii ya kufanya mikutano ya video inayoruhusu mawasiliano papo hapo na kushiriki maudhui ya kidijitali (picha, video na hati), na mawasiliano kupitia setilaiti.

2. **Ili kuhakikisha watu wote wakiwemo watu wenye ulemavu wanaweza kufikia, kuelewa na kutumia maelezo na huduma za kidijitali, vigezo vifuatavyo sharti vizingatiwe:**

    a. **Maelezo ya Umma** yaliyo katika muundo wa sauti na picha yanayotolewa kupitia skrini zilizo katika maeneo ya umma kama vile vituo vya treni, maduka ya rejareja, bustani na maneo mengine ya umma yanaweza kuwafikia watu wasio na vifaa binafsi vya kiteknolojia.[2] Ikiwezekana, sharti picha na michoro itumike pamoja na maandishi. Milio na/au ving'ora vinavyotumika wakati wa dharura sharti viandamane na taa zenye kumweka-mweka ili kuashiria aina na kiwango cha hatari.[3]

[2] *Idara ya Usafiri na Transport Scotland. Kanuni za Ufikivu wa Vituo vya Treni - Desturi za Utendakazi, ukurasa wa 109, K7. Ishara – skrini za matangazo.

[3] *Bodi ya Marekani Inayowashughulikia Watu wenye Ulemavu. 702 Mifumo ya Kutoa Habari Wakati wa Dharura

Maelezo na habari zinazotolewa kupitia Vipaza sauti vya Umma pia ziandamane na onyesho la kidigitali.[4]

b. **Redio** inaweza kutumika kwa kuongeza vipengele maalum au vifaa vya ziada ili ziweze kutumiwa na watu wasiosikia wenye matatizo ya kusikia. Kwa mfano, vifaa vinavyoweza kutoa matangazo kwa njia ya mtetemo, taa zinazowaka na maandishi mafupi ili kuwajulisha wasiosikia au wenye matatizo ya kusikia kuhusu kanuni na masharti yaliyowekwa na Serikali ili kuzuia kusambaa kwa COVID-19. Redio ya moja kwa moja ya mtandaoni au podcast sharti zijumuishe manukuu ya maudhui.[5]

c. **Televisheni:** Manukuu kwa lugha husika sharti yatolewe ili kufanya matangazo ya sauti kuhusu COVID-19 yaweze kufikiwa na watu wenye matatizo ya kusikia au wale wasioelewa lugha inayotumika. Isitoshe, sharti kuwepo na wakalimani wa lugha ya ishara wakati wa kutoa matangazo kwenye runinga kuhusu janga hili.[6]

d. **SMS:** Ikiwa ujumbe unatolewa tu kwa njia ya SMS, watu wanaohitaji vyanzo vya sauti na hawana vifaa mahiri vinavyoweza kubadilisha muundo wa ujumbe kuwa tofauti kama vile sauti hawatafikiwa na ujumbe. Hivyo basi, ilani na arifa kuhusu kanuni na tahadhari zinazohusu janga la COVID-19 sharti zitolewe kwa miundo tofauti kupitia njia mbalimbali. Picha zote zilizoambatishwa kwenye ujumbe sharti zijumuishe maelezo mbadala.

e. **WhatsApp** inaweza kutumiwa na watu wote na inatumia huduma ya Talkback na Voice Over. Programu ya Siri itasoma ujumbe wa WhatsApp kwa sauti na kwenye simu zinazotumia matoleo mapya ya programu, unaweza kuandika ujumbe kwa kutamka ukitumia programu ya Siri. Unapotumia WhatsApp epuka kutumia emoji.

f. Arifa za **Barua pepe** kuhusu COVID-19 sharti zitolewe kwa lugha nyingi. Programu inapaswa kusanidiwa kulingana na mwongozo wa ufikivu ili kuiwezesha kutumika bila hitilafu kwenye vifaa tofauti na kwa kujumuisha teknolojia ya kuwasaidia watu wenye ulemavu. Baadhi ya mifumo ya arifa za kompyuta ya mezani inaweza kuhakikisha kuwa ujumbe ibukizi unatolewa kwa njia tofauti kando na maandishi na milio.
Kutumia picha kwenye arifa za COVID-19 kunaweza kuwasaidia watu wanaotatizika kuelewa ujumbe wa maandishi. Picha zote sharti zijumuishe maelezo mbadala.[7]

---

[4] *Idara ya Usafiri na Transport Scotland. Kanuni za Ufikivu wa Vituo vya Treni - Desturi za Utendakazi, ukurasa wa 115, L1. Matangazo – ya jumla.

[5]*Baraza la Kitaifa kuhusu Ulemavu kwenye "Njia za Mawasiliano Zinazowafaa Watu wenye Ulemavu: Kabla, Wakati wa, na Baada ya Dharura". Ukurasa wa 45: Jinsi ya kuhakikisha ufikivu; ukurasa wa 104: Jedwali la 9. Njia za Kupokea na Kuthibitisha Arifa; ukurasa wa 148: Desturi Mpya: Matangazo ya Redio yenye Manukuu

[6] *Baraza la Kitaifa kuhusu Ulemavu. "Njia za Mawasiliano Zinazowafaa Watu wenye Ulemavu: Kabla, Wakati wa, na Baada ya Dharura". Ukurasa wa 45: Jinsi ya kuhakikisha ufikivu; ukurasa wa 104: Jedwali la 9. Njia za Kupokea na Kuthibitisha Arifa

[7] *Microsoft: Fanya huduma yako ya akaunti ya Outlook ifikiwe na watu wenye ulemavu

g. **Mitandao ya kijamii:** Matoleo mapya ya mitandao maarufu ya kijamii yanazidi kuwa rahisi kufikiwa. Hii ina maana kuwa, Facebook, Instagram, Twitter, YouTube zinatoa zana za ufikivu. Taasisi za kimatibabu na mawasiliano zinazochapisha kanuni na maelezo muhimu kuhusu janga la COVID-19 kwenye mitandao hii zinapaswa kufahamu kuhusu ufikivu wa maudhui ya kidijitali ili kuhakikisha kuwa yanafikiwa na watu wote.[8]

h. **Tovuti** zinazotoa maelezo kuhusu COVID-19 na maelezo mengine husika ili kuzuia msambao ulimwenguni / katika eneo au nchi fulani sharti ziwe zimekaguliwa ikiwa zina zana za ufikivu[9] ili kuhakikisha kuwa hakuna vizuizi kwa watu wenye ulemavu katika kufikia maelezo muhimu yaliyoshirikiwa kwenye tovuti. Hati zote husika za kidijitali (word, PDF) zinazotolewa kwenye tovuti zinaweza kufikiwa au kutofikiwa na watu wanaotumia visoma skrini ikiwa ziko katika miundo isiyosomeka kwa sauti, kama vile faili za JPEG au PDF zenye picha zisizosomeka (mf. picha zilizochanganuliwa).
Kwa upande mwingine, picha na michoro ni njia mwafaka zaidi za kuwasilisha maudhui kwa watu wenye ulemavu wa akili, au watu wanaotumia lugha tofauti; hata hivyo, sharti njia hii iambatane na maelezo yaliyotolewa kwa njia ya maandishi ili kuhakikisha kuwa wenye matatizo ya kuona wanaotumia programu ya sauti au inayosoma skrini ya breli wanaweza kupokea na kuelewa habari inayotolewa. Viungo vya tovuti za nje vinapaswa kuwa bainifu. Kila kipengee kwenye tovuti kinapaswa kiweze kufikiwa kwa kutumia kibodi kwa watu wasiotumia kipanya.[10]

Ili upate nyenzo na maelezo ya ziada ya ITU kuhusu kusaidia kujumuishwa kidijitali kwa watu wenye ulemavu, tafadhali tembelea: Ufikivu wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa Watu wenye Ulemavu na Ujumuisho wa Kidijitali wa ITU-D

---

[i] ***Mwongozo huu haujumuishi maelezo yote***
Kanusho la tafsiri Tunajitahidi kutoa tafsiri sahihi ya Mwongozo mfupi wa ITU kuhusu "*Jinsi ya kuhakikisha kuwa maelezo, huduma na bidhaa za kidijitali zinafikiwa na watu wote, wakiwemo Watu wenye Ulemavu wakati huu wa COVID-19*" kwa lugha nyinginezo kando na lugha 6 halisi zilizotumika za Shirika la Umoja wa Mataifa: Kiingereza , Kiarabu , Kichina , Kifaransa , Kirusi, Kihispania , hata hivyo, huenda kukawa na tofauti ndogo kati ya ujumbe halisi

---

[8]*Huduma ya Dijitali ya Serikali ya Uingereza. Mwongozo wa Mitandao ya Kijamii - Ufikivu
[9] *Kiwango cha kuhakikisha Ufikivu wa Maudhui kwenye Wavuti kulingana na WCAG 2.1

[10] *Mafunzo ya Mpango wa W3C wa Ufikivu wa Wavuti

*** Si nyenzo ya ITU:** *Maelezo yote kwenye tovuti hizi yametolewa kwa nia njema, hata hivyo hatutoi hakikisho, utangazaji au dhamana ya aina yoyote, iliyotajwa au iliyodokezwa kuhusu usahihi, utoshelevu, uhalali, kuaminika, upatikanaji au ukamilifu wa maelezo yaliyotolewa kwenye tovuti hizi za nje.*

na ujumbe uliotafsiriwa kutokana na matumizi ya msamiati maalum na kuwepo kwa tofauti katika maana za maneno. Hakuna kuwajibikia kutotaja, makosa, utata wowote kuhusu usahihi wa maelezo, au kuaminika kwa maelezo yaliyotafsiriwa. Endapo kuna mzozo, matoleo halisi ya Kiingereza yatatumika.